



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**  
**WIZARA YA AFYA**  
**TAARIFA KWA UMMA**

**MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 07/05/2020.**

Wizara ya Afya, Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya 29 wa Corona (COVID-19) nchini na kufikia idadi ya wagonjwa mia na thelathini na mne (134) kutoka wagonjwa mia na tano (105) ambao tuliovatolea taarifa siku ya tarehe 26 Aprili 2020. Wagonjwa wote wapya ni Raia wa Tanzania. Kati ya hao, wagonjwa 16 wanatoka Unguja na 13 Pemba.

Pia wagonjwa kumi na moja wamepona, hivyo kusanya jumla ya idadi ya wagonjwa walopona kufikia kumi na sita (16) hapa nchini.

Wizara inasikitika kutoa taarifa ya wagonjwa watano (5) ambao wamesariki dunia kutokana na ugonjwa wa Korona. Kwa niaba ya Serekali, Wizara inawapa pole wafisa na tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi.

Hadi leo wagonjwa ambao wamelazwa katika vituo vya kutolea huduma ni 41 na wanaendelea vizuri

Utaratibu wa kuwatibu wagonjwa wenye dalili chache majumbani na ambao hawana matatizo mengine ya kifaya unaendelea ambapo kwa sasa jumla ya wagonjwa 72 wanapata tiba majumbani na wakifutiliwa kwa karibu na wahudumu wa afya.

Serikali kupitia wizara ya Afya, inaendelea kuwasilitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji yakutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuhairisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima.

Aidha Wizara inasilitiza wananchi kuvali barakoa muda wote wanapotoka nje ya nyumba zao na wanapokuwa maeneo hatarishi kama sokoni, kwenye daladala, vituo vya afya na maeneo ya aina yote yenye mikusanyiko ya watu wengi.

Watu ambao wana dalili za homa kali, kikohozi na kupiga chafya kujitokeza wanaombwa kufika katika vituo vyetu vya afya au kupiga simu namba 190.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa huu wa COVID-19 kutoka wizara ya Afya.

Ndugu wananchi tuendelee kumuomba Mungu azidi kutulinda na kutuepusha na maradhi haya

.....  
Hamad Rashid Mohamed (MBM, MBLW)

Waziri wa Afya -Zanzibar